BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Thelathini na Tano – Tarehe 19 Juni, 2026

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Fedha na Mipango:**

Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Trilioni Nane, Bilioni Mia Tano Ishirini na Tano, Milioni Mia Nane Arubaini na Tisa, Laki Tano na Elfu Moja, Mia Saba Kumi na Nane, kwa Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia Siku ya Tarehe Thelathini Juni, Mwaka wa Elfu Mbili na Ishirini na Saba, Kuruhusu Utoaji na Uhaulishaji wa Fedha Hizo Pamoja na Mambo Yanayohusiana na Hayo.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

507. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Serikali imeanzisha Mabaraza ya Wilaya ya Watu Wenye Ulemavu, ili kuimarisha uratibu na utatuzi wa changamoto zinazowakabili katika ngazi ya jamii.

(a) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuyawezesha Mabaraza hayo kwa rasilimali na usaidizi wa kitaasisi, ili yaweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

(b) Je, ni hatua zipi zinazochukuliwa kujenga uwezo wa wanachama wa Mabaraza hayo, ikiwemo mafunzo na uongozi.

(c) Je, Serikali ina mfumo gani wa ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa Mabaraza hayo, ili kuhakikisha yanatekeleza majukumu yao ipasavyo.

## Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

435. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ:

Kuna magari ambayo yanasafirisha taka na kuzipeleka sehemu maalum iliyotengwa rasmi.

Je, ni mipango gani madhubuti imewekwa ya kuzisafirisha taka hizi bila ya kuathiri afya za wananchi kwa kuwakinga na harufu na kuzimwaga njiani wakati wa kuzisafirisha.

## Wizara ya Afya:

235. MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kabla ya kuja kwa makampuni binafsi katika Sekta ya Afya, wananchi wa Zanzibar walifurahia sana huduma, ukarimu, upole na hata utamaduni na heshima zao katika hospitali mbalimbali za Zanzibar, tofauti na hali ilivyo sasa baada ya huduma ya afya kubinafsishwa, wananchi hao wamekuwa wanapata dhiki isiyosemeka.

Ni ipi kauli ya Serikali kuhusiana na hali hii.

## Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

181. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kumekuwa na malalamiko ya wananchi wengi dhidi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati (ZURA), kwa kushindwa kusimamia Vituo vya Uzajishaji wa Nishati ya Mafuta kwenye vipimo.

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kwa vituo vya mafuta ili

kudhibiti ukamilifu wa lita, pindi wananchi wanapokwenda kupata huduma katika vituo hivyo.

(b) Kwa nini Serikali ilizihamisha kampuni za kizalendo zinazomilikiwa na wazawa katika *Depot* ya Mtoni na kumuwacha mgeni kwenye eneo hilo.

(c) Ni upi mpango wa Serikali katika kudhibiti ujenzi holela wa vituo vya mafuta hapa Zanzibar.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

163. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Nchi yetu sasa inakabiliwa na matukio na vitendo vingi vya unyanyasaji wa kijinsia na mpaka sasa Serikali haijaweka nguvu za kutosha katika kuanda na kuchukua hatua kali dhidi ya wafanyaji wa vitendo hivi.

(a) Je, Mswada wa Sheria ya Ustawi wa Jamii Zanzibar umefikia hatua gani.

(b) Je, Wizara ina maafisa wangapi wa Ustawi wa Jamii ambao hutoa huduma kwa jamii ya wazanzibari.

(c) Je, Serikali ina mahusiano gani na Chama cha Wataalamu wa Ustawi wa Jamii Zanzibar (ZASWA) katika kupambana na matukio haya.

**Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:**

343. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Kwa kuwa kuanzia mwaka 1987 mpaka 1992, kulikuwa na ujenzi wa Uwanja wa Gombani Pemba na Serikali iliajiri wazawa wapatao 92 kwa mkataba wa miaka 6.

(a) Je, Serikali inalijua suala hili kwa kiwango gani.

(b) Kwa nini mpaka leo wananchi hao 92 hawajalipwa stahiki zao licha ya kufuatilia maeneo mbalimbali kudai haki zao bila ya mafanikio.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

151. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Je, Serikali ina mikakati gani ya muda mrefu ya kupunguza ajali za barabarani na utekelezaji wake umefikia wapi.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

371. MHESHIMIWA SAID AZANA MSINGIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa hivi sasa, dunia inaelekea katika matumizi makubwa ya teknolojia, lakini bado tunashuhudia katika skuli zetu hasa za vijijini, wanafunzi wapo nyuma katika matumizi ya teknolojia.

Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kunakuwa na matumizi ya teknolojia ya kisasa katika kufundishia.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

505. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (JIMBO CHAKE CHAKE) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Majengo ya kihistoria ni sehemu muhimu katika kulinda historia, urithi wa taifa na kukuza utalii. Zanzibar imebahatika kuwa na majengo mengi ya kihistoria, yenye thamani kubwa ya kiutamaduni na kiuchumi.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuyatambua rasmi majengo ya kihistoria yaliyopo Zanzibar.

(b) Je, ni hatua zipi zinazochukuliwa kuyahifadhi na kuyatunza majengo hayo, ili yaendelee kuwa sehemu ya urithi wa taifa.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

287. MHESHIMIWA ALLEY MASOUD ALLEY (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kwa kuwa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar ndio taasisi inayosimamia huduma za Mahujaji kupitia mashirika mbalimbali. Na kwa kuwa kwa muda mrefu sasa kumekuwepo na malalamiko ya baadhi ya Mahujaji kutoka Tanzania bara kutumia huduma zinazogharamiwa na Mahujaji wa Zanzibar bila ya kuchangia.

Je, Serikali imejipanga vipi kushughulikia kero hiyo ili kuhakikisha haki na usawa kwa Mahujaji wote.

**III. HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Fedha na Mipango:**

Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Trilioni Nane, Bilioni Mia Tano Ishirini na Tano, Milioni Mia Nane Arubaini na Tisa, Laki Tano na Elfu Moja, Mia Saba Kumi na Nane, kwa Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia Siku ya Tarehe Thelathini Juni, Mwaka wa Elfu Mbili na Ishirini na Saba, Kuruhusu Utoaji na Uhaulishaji wa Fedha Hizo Pamoja na Mambo Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa mara ya Pili.

**Zanzibar,**
**19 Juni, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR.**